

Nikitumia nyembe kali au sindano pamoja na mtu mwenye Virusi vya UKIMWI ninaweza kupata Virusi vya UKIMWI na UKIMWI?

By SW - Melkisedeck Shine · April 17, 2022

Ujana na Makuzi | Mapenzi na Ngono Salama

Ndiyo, unaweza kuambukizwa ukitumia nyembe kali au sindano kwa kuchangia pamoja na mtu mwenye virusi vya UKIMWI. Matumizi ya vyombo vyenye makali, kama sindano, visu au nyembe yana hatari. Kama baada ya kutumika damu husalia katika vyombo hivi, na endapo vitatumika bila kutakaswa au kuchemshwa, matumizi yake yanaweza kusababisha maambukizi ya magonjwa mbalimbali, pamoja na UKIMWI. Kwa hiyo ni muhimu sana kutochangia vifaa vyenye makali na watu wengine au lazima kuvitakasa na kuchemsha kila baada ya kuvitumia.

Printable AckySHINE Article · <https://ackyshine.com/post.php?post=25897>